**WATETEZI WA KISWAHILI UGANDA – WAKIU**

"Kiswahili Nguvu Yetu"

+256 788 820 020
+256 703 533 033

Address: P. O Box 171820, Kampala, Uganda.
Email: wateteziuganda@gmail.com

## TAARIFA FUPI YA KAMATI YA MPITO

Heri ya mwaka mpya kwenu nyote!

Pokeeni, salamu kutoka kamati ya mpito ya Watetezi wa Kiswahili Uganda – WAKIU. Awali ya yote tunamshukuru Mungu kwa kutulinda na kutuwezesha kusukuma gurudumu la kukikuza na kukiendeleza Kiswahili katika nyanja mbalimbali nchini.

Salamu za pole ziwafikie wote waliopoteza wapendwa wao. Hususani, tuendelee kuwakumbuka kwa sala walimu wenzetu waliotutoka mwezi Desemba, 2024. Mungu azidi kuwafariji wanafamilia na roho za marehemu zipumzike kwa amani.

Ikumbukwe kwamba harakati za WAKIU zilianza rasmi mnamo tarehe 25, mwezi Julai, 2024. WAKIU kilianza kama kikundi cha mtandaoni kupitia Whatsapp, ambamo walimu na wataalamu mbalimbali wa Kiswahili nchini walijiunga na kuanza kujadili masuala muhimu ya jinsi ya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili na fasihi nchini Uganda.

Kikundi hiki, kwa sasa kinaongozwa na kamati ya mpito. Kamati hiyo ni kama ifuatayo;

| | | |
|---|---|---|
| i. | Bi. Loyce Kemigabo | (Mwenyeketi) |
| ii. | Bw. Simon Twijukye | (Katibu Mkuu) |
| iii. | Bw. JohnPaul Arigumaho | (Katibu Mwenezi) |
| iv. | Bi. Eve Owembabazi | (Mhazini) |
| v. | Bi. Angella Komushana | (Mhazini Msaidizi) |
| vi. | Bw. Joseph Tusingwire | (Mjumbe) |
| vii. | Bw. Micah Bamugyeya | (Mjumbe) |
| viii. | Bi. Skylet Mmboga Mbecha | (Mjumbe) |
| ix. | Bw. Preston Bahati | (Mjumbe) |
| x. | Bw. Johnson Muhindo | (Mjumbe) |
| xi. | Bw. Innocent Agume | (Mshauri) |
| xii. | Dkt. Caesar Jjingo | (Mshauri) |
| xiii. | Dkt. Asiimwe Caroline | (Mshauri) |
| xiv. | Bw. Patrick Kaboyo | (Mlezi) |

Kamati hiyo kwa kupitia vikao vyake vya ana kwa ana na mtandaoni, imefanikiwa kujadili masuala yanayohusu utetezi na watetezi (hasa walimu) wa Kiswahili na namna ya kukuza na kukiendeleza Kiswahili hasa nchini Uganda.



WATETEZI WA KISWAHILI UGANDA (WAKIU)
30 JAN 2025

Kwa mantiki hiyo, kamati ya mpito imefanikiwa kutekeleza yafuatayo;

i. Kupata dira, dhamira na malengo mahususi ya WAKIU. Haya yote yapo bayana kwenye katiba ya WAKIU, na yatabainishwa ipasavyo kwenye tovuti ya chama.

ii. Mchakato wa kuandaa katiba ya chama ulianza na kukamilishwa. Kutoka mifukoni mwa wanakamati wa kamati ya mpito walikusanya zaidi ya shilingi milioni moja kufanikisha zoezi la katiba lililoratibiwa na mwanasheria, ndugu Ronald Kironde wa Musisi Kironde Legal.

iii. Hatua za kusajili WAKIU zilikamilika pia. Sasa hivi WAKIU kinatambulika rasmi ndani na nje ya nchi. Hatua nyingine zilizofanikishwa ni pamoja na; kutengeneza muhuri na nembo rasmi ya WAKIU bila kusahau namba ya sanduku la posta.

iv. Ufunguzi wa akaunti ya benki ya WAKIU kupitia Benki ya Posta Uganda upo katika hatua za mwisho. Hili pia linatekelezwa na fedha zilizokusanywa kutoka kwa wanakamati wa kamati ya mpito.

**MIPANGO YA MWAKA 2025**

i. Kamati ya mpito ya WAKIU itaendelea kuwahimiza walimu wote wa Kiswahili kujisajili katika orodha ya kitaifa. Hili litawasaidia wengi kuwa tayari kwa fursa yoyote kupitia Wizara ya Elimu na Michezo. Aidha, mnapaswa kujisajilisha pia kwenye mfumo wa wizara wa Teacher Management Information System (TMIS) https://tmis.go.ug/, ili kutimiza vigezo vya awali vya kuajiriwa serikalini. Shukurani za dhati kwa ndugu Innocent Agume kwa kujitolea na kuhakikisha orodha hiyo inahuishwa kila wakati.

ii. Kuzindua rasmi chama cha Watetezi wa Kiswahili Uganda (WAKIU). Uzinduzi huu umepangwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Machi au mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2025.

iii. Vilevile kuna mpango wa kutembelea ofisi mbalimbali kukutana na maafisa wa ngazi tofauti. Lengo la ziara hizi ni kuwaweka viongozi hawa katika mstari wa mbele kutambua shughuli za WAKIU hususani kukitetea na kukikuza Kiswahili nchini.

iv. Mpango wa maandalizi ya kuadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani (tarehe 7, mwezi Julai, 2025) yanatarajiwa kuanza mapema punde tutakapohitimisha ufunguzi wa akaunti ya benki.

v. Kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa Kiswahili kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile televisheni, redio na magazeti. Kwa upekee ningependa kumshukuru Dkt. Caesar Jjingo wa Chuo Kikuu cha Makerere, kwa makala zake anazoandika magazetini kuwa ni za muhimu na zinaleta mawazo chanya kwa wengi. Aidha, shukrani



WATETEZI WA KISWAHILI UGANDA (WAKIU)

za dhati kwa ndugu Nyachwara Edwin wa Televisheni ya Taifa (UBC) kwa fursa anazotupatia WAKIU, bila kumsahau Ndugu John Paul, msemaji wa kamati ya mpito, kwa kuielimisha jamii kila wakati.

vi. Suala la kuanzisha tovuti ya WAKIU halijasahaulika. Tovuti hiyo itazinduliwa rasmi ndani ya wiki chache zijazo baada ya kukamilika. Kupitia tovuti ya WAKIU, taarifa kuhusu Kiswahili zitawekwa bayana zikiwemo; Uongozi na bodi ya WAKIU, orodha ya wanachama hai wa WAKIU, mitihani ya Kiswahili kutoka majimbo/kanda mbalimbali ndani na nje ya nchi, habari kuhusu makongamano. Bila kusahau, taarifa ibuka kuhusu lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Tovuti pia itahifadhi rasilimali na takwimu mbalimbali kwa ajili ya kupakuliwa na jamii ya Waswahili ndani na nje ya nchi.

vii. Pia ni mpango na lengo la muda mrefu la WAKIU kusaidiana katika shida na raha. Mkutano mkuu utatoa maelekezo zaidi juu ya hili kwa mujibu wa katiba ya WAKIU. Ningependa pia kuwashukuru Bi. Eve Owembabazi na Bi. Angella Komushana kwa kutuongoza bila kuchoka katika kuratibu shughuli hizi wakati wote zitokeapo.

Mabibi na mabwana, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru wote kwa jitahada zenu za kutetea Kiswahili tangu kuasisiwa kwa WAKIU. Bila kusahau, ninawashukuru wanakamati wenzangu wa kipindi hiki cha mpito kwa kujitolea kwao kwa namna moja ama nyingine.

Asanteni sana na Mungu awabariki.

Ndimi,

WATETEZI WA KISWAHILI UGANDA (WAKIU)
30 JAN 2025
KISWAHILI NGUZO YETU

..........................................

SIMON TWIJUKYE

**KATIBU MKUU (KAMATI YA MPITO)**

30 Januari, 2025.